Iweni Za Biblia
(Bible Be’s)

Na

Ellis P. Forsman

Iweni Za Biblia

Na

Ellis P. Forman

Octoba 11, 2011

Iweni Za Biblia

Efe. 4:32-5:21

Biblia inafunua idadi ya "Iweni" ambayo itakuwa sehemu ya maisha ya kila Mkristo.

Iweni wakarimu

Hapa kuna kutiwa moyo inayohitajika kwa kila Mkristo.

Efe. 4:32, "*Tena iweni wafadhili ninyi kwa ninyi, wenye huruma mkasameheane kama na Mungu katika Kristo alivyowasamehe ninyi.*"

Hii ni kuhesabu matatizo yalipo katika nafsi ya mwanadamu. Efe. 4:31, "*Uchungu wote na ghadhabu na hasira na kelele na matukano yaondoke kwenu, pamoja na kila aina ya ubaya.*"

Makanisa yamegawanyika, urafiki umevunjika, miji imeshidwa kwa sababu ya kukosa ukarimu.

Ukarimu unajumuishwa ndani msamaha, kama ilivyoonyeshwa katika Waefeso 4:32 hapo juu.

Ukarimu pia ujumuishwa ndani ya upendo. 1 Kor. 13:4, "*Upendo huvumilia, hufadhili, upendo hauhusudu; upendo hautakabari; haujivuni;*"

Ukarimu ni moja kati ya rehema za Mkristo. 2 Petro 1:7, "*Na katika utauwa wenu upendano wa ndugu, na katika upendano wa ndugu, upendo.*"

Iweni na kiasi

Hii haimanishi kama inavyotafsiriwa kwa kiingereza leo (sio kuzidiwa na kilevi).

Inamaanisha kuweka akili yako katika kumanisha; hata kama kilevi kinaweza kuathiri akili yenye maantiki.

- **Kuwa tayari kumpiga vita Shetani.** 1 Pet. 5:8, "*Mwe na kiasi na kukesha kwa kuwa mshitaki wenu Ibilisi kama samba angurumaye, huzunguka zunguka akitafuta mtu ammeze.*"
- **Kuwa tayari kwa kazi iliyopo mikononi mwetu.** 1 Pet. 1:13, "*Kwa hiyo vifungeni viuno vya nia zenu na kuwa na kiasi; mkiitumainia kwa utimilifu ile neema mtakayoletewa katika ufunuo wake Yesu Kristo.*"

- **Tusaidie kuomba.** 1 Pet. 4:7, "*Lakini mwisho wa mambo yote umekaribia; basi, iweni na akili mkeshe katika sala.*"
- **Tusaidie kukesha, kuwa tayari.** 1 Thes. 5:6, "*Basi tusilale usingizi kama wengine, bali tukeshe na kuwa na kiasi.*"

Hili neno ni muhimu sana "iweni" za Biblia.

Toshekeni

Paulo alijifunza kutosheka bila kujali hali yoyote ya duniani. Fil. 4:11, "*Si kwamba nasema haya kwa kuwa nina mahitaji; maana nimejifunza kuwa radhi na hali yo yote niliyo nayo.*"``

Mwanadamu haridhiki na asili. Kadiri anavyopata zaidi, ndivyo anavyo hitaji.

Paulo hapendekezi uvivu.

- 1 Thes. 4:11, "*Tena mjitahidi kutulia na kutenda shughuli zenu, na kufanya kazi kwa mikono yenu wenyewe kama tulivyowaagiza.*"
- 2 Thes. 3:10, "*Kwa kuwa hata wakati ule tulipokuwapo kwenu tuliwaagiza neno hili, kwamba ikiwa mtu hataki kufanya kazi, basi asile chakula.*"

Afadhali, utosheke baada ya kutenda kilicho chema.

Kuridhika kunatusaidia kushukuru.

- 1 Tim. 6:8, "*Ila tukiwa na nguo na chakula tutaridhika na vitu hivyo.*"
- Heb. 13:5, "*Msiwe na tabia ya kupenda fedha, , mwe radhi na vitu mlivyonavyo, kwa kuwa yeye mwenyewe amesema; Sitakupungukia kabisa wala sitakuacha kabisa.*"

Mafanikio makubwa ya mwanadamu: utauwa na kuridhika. 1 Tim. 6:6, "*Walakini utauwa pamoja na kuridhika ni faida kubwa.*"

Iweni hodari

Kabla ya kutoa silaha za Ukristo, Paulo anasema: Efe. 6:10, "*Hatimaye mzidi kuwa hodari katika Bwana na katika uweza wa nguvu zake.*"

Mungu ni hodari. Pia anapenda watoto wake wawe hodari ili kuweza kumshinda Shetani.

Mkristo anapata nguvu zake kutoka kwa Mungu. Paulo alimsihi Timotheo kuwa hodari. 2 Tim. 2:1, "*Basi wewe mwanangu uwe hodari katika neema iliyo katika Kristo Yesu.*"

Tunapaswa kuwa hodari ili tusianguke. 1 Kor. 16:13, "*Kesheni, simameni imara katika imani, fanyeni kiume mkawe hodari.*"

Kuwa Samsoni wa kiroho kwa ajili ya Bwana.

Iweni tayari

"Tayari" katika Agano Jipya inamanisha "kujiandaa".

Paulo alijiandaa. 2 Tim. 4:6, "*Kwa maana mimi sasa namiminwa, na wakati wa kufariki kwangu umefika.*"

Huu ndio wakati pekee tuliopewa ili kuwa tayari kwa ajili ya Hukumu.

Ni wale tu waliotayari ndio watakaoingia mbinguni. Mat. 25:1-13, "*Ndipo ufalme wa mbinguni utakapofanana na wanawali kumi, walio twaa taa zao, wakatoka kwenda kumlaki bwana arusi. Watano kati yao walikuwa wapumbavu, na watano wenye busara. Wale waliokuwa wapumbavu, walizitwaa taa zao, wasitwae na mafuta pamoja nao; bali wale wenye busara walitwaa mafuta katika vyombo vyao pamoja na taa zao. Hata bwana arusi alipokawia, wote wakasinzia wakalala usingizi. Lakini usiku wa manane pakawa na kelele, haya bwana arusi tokeni mwende kumlaki. Mara wakaondoka wanawali wale wote, wakazitengeneza taa zao. Wale wapumbavu wakawaambia wenye busara, tupeni mafuta yenu kidogo maana taa zetu zinazimika. Lakini wale wenye busara wakawajibu, wakisema, sivyo; hayatatutosha sisi na ninyi; afadhali shikeni njia mwende kwa wauzao, mkajinunulie. Na hao walipokuwa wakienda kununua bwana arusi akaja, nao waliokuwa tayari wakaingia naye arusini; mlango ukafungwa. Halafu wakaja na wale wanawali wengine, wakasema, Bwana, Bwana, utufungulie. Akajibu akasema, amin nawaambia siwajui ninyi. Basi kesheni kwa sababu hamwijui siku wala saa.*"

Tunapaswa kuwa tayari kutetea neno la Mungu

1 Pet. 3:15, "*Mwe tayari siku zote kumjibu kila mtu awaulizaye habari ya tumaini lililo ndani yenu; lakini kwa upole na kwa hofu.*"

Kuwa tayari kwa ajili ya vita na shetani.

Petro alidhani alikuwa tayari kupigana na Shetani, lakini hakuwa tayari. Luka 22:31-34, "*Tena kwa habari ya kiyama ya watu, hamjalisoma neno lililonenwa na Mungu, akisema mimi ni*

Mungu wa Ibrahimu, na Mungu wa Isaka, na Mungu wa Yakobo? Mungu si Mungu wa wafu, bali wa walio hai. Na makutano waliposikia wakashangaa kwa mafunzo yake."

1 Pet. 5:8, "*Nanyi vumilieni, mthibitishe mioyo yenu, kwa maana kuja kwake Bwana kunakaribia.*"

Vumilia; kuwa hodari; kuwa tayari kwa ajili ya kazi. Tito 3:1, "*Uwakumbushe watu kunyenyekea kwa wenye uwezo na mamlaka, na kutii, na kuwa tayari kwa kila kazi njema.*"

Kuwa tayari kwa kila saa kwa sababu hatujui wakati wa kuja kwake. Mat. 25:13, "*Basi kesheni, kwa sababu hamwijui siku wala saa.*"

Iweni waminifu

Wale watakaokutwa wakiwa waaminifu watapokea uzima. Ufu. 2:10, "*Usiogope mambo yatakayokupata; tazama huyo Ibilisi atawatupa baadhi yenu gerezaani ili mjaribiwe, nanyi mtakuwa na dhiki siku kumi. Uwe mwaminifu hata kufa, name nitakupa taji ya uzima.*"

Wengi huanza mbio, lakini hushindwa. Ni waaminifu pekee ndio watapokea taji ya uzima. Paulo aliendelea kwa ajili ya Bwana. 2 Tim. 4:6, "*Kwa maana mimi sasa namiminwa, na wakati wa kufariki kwangu umefika.*"

Waaminifu watapewa zawadi. Mat. 25:21, "*Bwana wake akamwambia Vema, mtumwa mwema na mwaminifu; ulikuwa mwaminifu kwa machache; nitakuweka juu ya mengi; ingia katika furaha ya bwana wako.*"

Hitimisho

Je hizi "Iweni Za Biblia" ni sehemu ya maisha yako? Zinawakilisha maonyo yanayofaa kukubalika. Je! Uko upande wa Bwana? Kama siyo, kwa nini usimkubali Yesu na misingi yake ili "Uwe" katika umilele na uwepo wake.

- **Imani.** Waeb. 11:6, *"Lakini pasipo imani haiwezekani kumpendeza; kwa maana mtu amwendeaye Mungu lazima aamini kwamba yeye yuko, na kwamba huwapa dhawabu wale wamtafutao."* Nilipokuwa shuleni (nikiwa na miaka 17), kijana mmoja jirani yangu mwaka sawa na mimi akniambia kwamba haamini kwamba Mungu yuko. Kwa vile nilisha batizwa, nilichukua nafasi ya kuongea naye kuhusu mandiko. Akaniambia kwamba anaweza kuona kwamba kuishi maisha ya ukristo ni nzuri, lakini hakuwa na uhakika

kwamba Mungu yuko. Lakini ili kuwa upande salama, labda anapaswa kwenda kanisani, na akifa na kusimama mbele za Mungu (kama kuna Mungu) siku ya hukumu (kama kuna hukumu), labda kama Mungu akiona kuwa amekwenda kanisani atampeleka mbinguni (kama kuna mbingu), na si motoni (kama kuna moto). Nikamwambia, "haifanyi kazi kwa njia hiyo. Lazima uamini katika yeye kwa moyo wako wote la sivyo huwezi kumpendeza.

- **Toba.** Matend. 2:38, *"Petro akawambia, tubuni mkabatizwe kila mmoja wenu kwa jina lake Yesu Kristo kwa ajili ya ondoleo la dhambi zenu nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu."* Matend 11:18, *".....Basi Mungu amewajalia hata mataifa nao toba liletalo uzima."* Kama ulikuwa unalala, ukasikia kelele kwenye chumba kingine, na unafikiria mwenyewe, "Kwamba kuna mwizi!" taratibu unachukua simu ya mkononi, unawapigia polisi. Kidogo polisi wanafika na kumshika mwizi. Alafu anapiga kelele, "samahani; samahani!" Anaomba msamaha wa nini? Kwa sababu amekamatwa; si kwamba ameiba. Toba iliyokweli ni kwamba mwizi angeomba msamaha kwamba hataiba tena. Hiyo ndio toba ya kweli. Ni badiliko la nia linaloleta badiliko la matendo. Tunatakiwa kufanya hivyo kabla hatujawa wakristo.

- **Kukiri.** Waru. 10:9-10, *"Kwa sababu ukimkiri Yesu kwa kinywa chako ya kuwa ni Bwana na kuamini moyoni mwako ya kuwa Mungu alimfufua katika wafu, utaokoka. Kwa maana kwa moyo mtu huamini hata kupata haki, na kwa kinywa hukiri hata kupata wokovu."* Tuna kiri nini? Kwamba tuna amini kwamba Yesu Kristo ni mwana wa Mungu.

  Kumbuka kwamba katika andiko hilo hapo juu kwamba imani (kuamini), toba, na kukiri ni "**KATIKA**" haki, uzima, au wokovu. "Katika" inamanisha kuelekeza kwenye kitu Fulani; si kwamba mtu ameshapata.

- **Ubatizo.** Ni katika ubatizo ndipo haki, uzima, na wokovu vinapatikana. Yesu mwenyewe alibatizwa kuitimiza haki yote, *"Lakini Yohana alitaka kumzuia akisema, mimi nahitaji kubatizwa na wewe, nawe waja kwangu? Yesu akajibu akamwambia kubali hivi sasa, kwa kuwa ndivyo itupasavyo kuitimiza haki yote. Basi akamkubali. Naye Yesu alipokwisha kubatizwa mara akapanda kutoka majini, na tazama mbingu zikamfunukia akamwona Roho wa Mungu akishuka kama hua, akija juu yake; na tazama sauti kutoka mbinguni ikisema,*

huyu ni mwanangu mpendwa, ninaye pendezwa naye." (Math. 3:14-17). Yesu alibatizwa kwa sababu Mungu alisema ni jambo sahihi la kufanya. Unaona ni jinsi gani ilivyompendeza Mungu Yesu alipobatizwa? Yesu pia akasema, "*Imekuwa kwetu **sisi** kuitimiza haki yote."* Tuna batizwa kwa sababu inatimiza haki yake yote, si kwa sababu ni haki yetu.

Kwa kweli, tusipo batizwa, tungali katika dhambi zetu. *"Petro akawambia, tubuni mkabatizwe kila mmoja wenu kwa jina lake Yesu Kristo kwa ajili ya ondoleo la dhambi, na mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu."* (Matend. 2:38). Petro, umesema kusudi la ubatizo ni nini? "*Kwa ajili ya ondoleo la dhambi*". Kwa nini watu wanapenda kuach hatua inayotuondoa dhambi zetu?

Yesu aliamuru kwamba ili kuufikia wokovu lazima tubatizwe. *"Na akawambia enendeni ulimwenguni kote mkahubiri injili kwa kila kiumbe. Aaminiye **na** kubatizwa ataokoka; asiyeamini atahukumiwa."* (Marko 16:15-16).

Anania alimwambia Sauli (kabla hajaitwa Paulo) kitu iki hiki, "*Unakawilia nini? Simama, na ubatizwe, na uoshwe dhambi zako, ukiliitia jina la Bwana."* (Matend. 22:16). Ubatizo ni hitaji lililotolewa na Mungu.

Ubatizo unaitwa maziko, *"Basi tulizikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo katika mauti yake kusudi kama Kristo alivyofufuka katika wafu kwa njia ya utukufu wa Baba, vivyo hivyo na sisi tuenende katika upya wa uzima."* (Waru. 6:4). Utu wetu wa kale umekufa. *"Hamfahamu ya kuwa sisi sote tuliobatizwa katika Kristo Yesu tulibatizwa katika mauti yake. Basi tulizikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo katika mauti yake, kusudi kama Kristo alivyofufuka katika wafu kwa njia ya utukufu wa Baba, vivyo hivyo na sisi tuenende katika upya wa uzima. Kwa maana kama mlvyounganika naye katika mfano wa mauti yake, kadhalika mtaunganika katika mfano wa kufufuka kwake; mkijua neno hili ya kuwa utuwetu wa kale ulisulubishwa pamoja naye, ili mwili wa dhambi ubatilike, tusiitumikie dhambi tena."* (Waru. 6:3-6). Ubatizo ni ramani ya Mungu inayotumiwa na damu ya Kristo katika maisha yetu kwa ubatizo. Tunakuwa huru na dhambi zetu za zamani kama tu tukibatizwa.

Hii haimanishi "kunyunyiza. Andiko hilo hapo juu linasema ubatizo ni maziko. Hatuwezi kupeleka maiti makaburini, na kumwekea udongo kidogo juu yake; tunauzika mwili.

Kama hujafanyika Mkristo, kwa nini usizingatie leo?